




TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA (TARI)

MAGONJWA SUMBUFU KATIKA ZAO LA MPUNGA

Magonjwa Muhimu ya Zao la Mpunga Tanzania



**Ukungu mkuu
(Rice blast)**



**Baka kahawia
(Rice Brown Spot)**



**Kimyanga
(Rice Yellow Mottle Virus Disease)**



**Mnyauko wa majani wa Bakteria
(Bacterial Leaf Blight)**

Mbinu za kudhibiti ugonjwa:

1. Ukungu mkuu

- Tumia mbegu zenye ukinzani
- Kutumia mbolea ya Nitrogen (Urea) kwa kiasi sahihi
- Furisha maji shambani mara kwa mara
- Safisha shamba kuondoa magugu na maotea
- Tumia viuatilifu (fungicide)
- Tumia mzunguko wa mazao ulio sahihi

2. Baka kahawia

- Tumia mbegu zenye ukinzani
- Zingatia matumizi sahihi ya mbolea
- Hakikisha shamba lina unyevu muda mwingi
- Weka shamba katika hali ya usafi
- Ongeza rutuba ya shamba kwa kuongeza virutubisho

3. Mnyauko wa majani wa Bakteria

- Tumia mbegu zenye ukinzani
- Usitumie kiasi kikubwa cha mbolea za naitrojeni
- Hakikisha usafi wa shamba kwa kuondoa magugu
- Tengeneza njia za kutolea maji wakati wa mafuriko
- Tumia viuatilifu vinavyopendekezwa kitaalamu

4. Kimyanga

- Tumia mbegu zenye ukinzani
- Ondoa magugu yanayoweza kuwahifadhi wadudu wasambazaji
- Ondoa mimea iliyoambukizwa na kuiteketeza
- Usishike mimea mingine baada ya kushika mimea iliyoambukizwa
- Tumia vifaa visafi ambavyo havijagusa maeneo yenye ugonjwa



@Tari tv



@Tari Tanzania



@tari

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:

Meneja wa Kituo

TARI Dakawa

S.L.P 1892, Morogoro, Tanzania

Simu: (+255) 23 2934300,

Baruapepe: cmdakawa@tari.go.tz